JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU KOROGWE**

Simu 027 2640540
027 2640847
Fax: 027 2640999
Email: korogwetc@moe.go.tz

S. L. P. 533
**KOROGWE.**

**03/06/2026**

Kumb. Na. KTC/Reg/Vol.1/123/18

Ndugu.........................................

S.L.P. ..........................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

## 1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukujulisha kuwa **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia** imekuchagua kujiunga na mafunzo ya **Stashahada Maalumu ya Ualimu Elimu ya Msingi Masomo ya Sayansi na Hisabati na Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa njia ya masafa** katika chuo hiki kwa mwaka wa masomo **2026/2027. Hongera sana.**

Stashahada Maalumu ya Ualimu Elimu ya Msingi mchepuo wa Sayansi na Hisabati ni kozi ya miaka **mitatu (3)** kwa wahitimu wa kidato cha nne na Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa Njia ya Masafa Mchepuo wa Sayansi ya Jamii na Lugha ya Kiswahili (Kwa kutumia Lugha ya Kiswahili) ni kwa walimu wenye Astashahada (**Cheti**) walio kazini na wale ambao bado hawajaajiriwa ni kozi ya **miaka (3-4)**. Ufafanuzi zaidi kuhusu masomo na mitihani yatatolewa wakati wa maelekezo kabilishi (Orientation Course) ambayo hutolewa kwa wanachuo wote wiki ya kwanza baada ya kuripoti chuoni.

## 2. TAREHE YA KURIPOTI CHUONI

Unatakiwa kuripoti chuoni tarehe **17.08.2026** ambapo baadae kutatolewa maelekezo (orientation) yahusuyo kozi yako na maisha ya chuoni.

## 3. MAHALI CHUO KILIPO

Chuo cha Ualimu Korogwe kipo katika wilaya ya Korogwe mkoa wa Tanga, kilometa mbili na nusu (Km 2.5) kutoka stendi mpya ya mabasi Korogwe mjini. Ukishuka kwenye basi tafuta bajaji zinazoelekea Hospitali ya Wilaya ya Korogwe (HOSPITALI YA MAGUNGA). Ukipenda unaweza kukodi Taxi au Bajaji ili ufike chuoni haraka. (kukodi usafiri wa bajaji nauli ni shilingi elfu moja na mia tano tu hadi chuoni). Usitumie usafiri wa bodaboda ni hatari kwa usalama wako.

## 4. MAHITAJI MUHIMU

### 4.1 Maagizo ya Vyeti/Nyaraka

i. Vyeti vyote **halisi vya kitaaluma** (Original Academic Certificates) vya Baraza la Mitihani la Tanzania Kidato cha **NNE (CSEE)**/vyeti vya kidato cha sita kwa wahitimu wa kidato cha sita na Vyeti vya Astashahada (Cheti) ya Ualimu kwa Walimu kazini au kwa waliohitimu astashahada (Cheti) ya ualimu.

ii. Vyeti vya kuhitimu Elimu ya Sekondari kidato cha NNE/Astashahada (Cheti) ya Ualimu (**Leaving Certificates**).

iii. Vivuli vya vyeti vya kidato cha **NNE/Astashahada(photocopy)**. Vyeti halisi vya taaluma vitabakia ofisi ya usajili kwa ajili ya uhakiki zaidi wa NECTA.

iv. Kibali cha kuruhusiwa kushiriki mafunzo kutoka kwa Mwajiri (Hii itawahusu walimu kazini walioajiriwa tu.

v. Cheti halisi cha kuzaliwa (**Birth Certificate**).

### 4.2 Ada ya Mafunzo

Ada ya mafunzo kwa mwaka ni Shilingi **450,000/=**. Ada hii inaweza kulipwa yote au kwa awamu mbili yaani kwa kila muhula. Malipo yafanyike kupitia mfumo wa malipo ya serikali kwa kutumia ***Control Number*** ambayo inapatikana Chuoni ofisi ya Mhasibu wa Chuo. Aidha, unaweza kuomba "Control Number" na ukalipa ada ukiwa nyumbani kwa kupiga simu zilizopo kwenye kipengele **Na.7.**

### 4.3 Michango Mingine

#### 4.3.1. Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi masomo ya Sayansi na Hisabati

| Na. | Mchango | Kiasi(Tsh) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Ulinzi | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 2. | Ukarabati | 25,000/= | Kwa mwaka |
| 3. | Kitambulisho na Usajili | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 4. | Kukodisha Godoro | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 5. | Vifaa vya Usafi na Mazingira | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 6. | Huduma ya kwanza | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 7. | Michezo | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 8. | Serikali ya Wanachuo | 5,000/= | Kwa mwaka |
| 9. | Bima ya Afya (Wasio na Bima) | 50,400/= | Kwa mwaka |
| | **JUMLA** | **200,400/=** | |

#### 4.3.2. Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa Njia ya Masafa

| Na. | Mchango | Kiasi(Tsh) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Ukarabati | 25,000/= | Kwa mwaka |
| 2. | Kitambulisho na usajili | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 3. | Huduma ya Kwanza | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 4. | Uendeshaji na ufuatiliaji wa mafunzo | 40,000/= | Kwa mwaka |
| 5. | Vifaa vya usafi mazingira | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 6. | Michezo | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 7 | Serikali ya Wanachuo | 5,000/= | Kwa mwaka |
| | **JUMLA** | **150,000/=** | |

Michango yote ambayo jumla yake ni Tsh. **200,400/= au 150,000/=** zilipwe kwenye akaunti ya Chuo **NMB** yenye jina **PRINCIPAL KOROGWE T.C ACCOUNT No. 41501100012** na kuwasilisha *Pay in Slip* yenye jina halisi la Mwanachuo.

**Muhimu:** Fedha ya matumizi binafsi au Fedha ya **Ada** isichanganywe na fedha ya michango.

**4.4 Maagizo ya Vifaa vingine kwa wote**

- Shuka mbili za rangi ya bluu bahari (Light blue).
- Koti jeupe la maabara (Lab coat) kwa watakaosoma masomo ya sayansi.
- Madaftari tisa (09) (**counter book quire 4**).
- Bunda moja la karatasi za fotokopi (**A4**) kwa mwaka.
- Chandarua (neti) ya kuzuia mbu.
- Ndoo ya kutunzia maji ya matumizi yako chumbani.
- Picha: Lete picha mbili (2) passport size light blue background.
- Vifaa vya chakula; bakuli, sahani, kijiko na kikombe.

**5. SARE YA CHUO:**

**Wanachuo wa Kike:**

i. Sketi mbili nyeusi zisizo za kubana na ziwe ndefu kiasi cha kuvuka magoti (Kipimo cha urefu kiwe usawa wa goti na kisigino). Kila moja iwe na rinda boksi lenye muonekano wa **V** kuelekea chini) (**Tazama mchoro ukurasa wa 6.**

ii. Mashati mawili ya mikono mirefu ya bluu bahari (light blue) na koti jeusi.

iii. Kwa wasichana wa kiislam watavaa suruali rangi nyeusi na nusu kanzu (Punjab) rangi ya bluu bahari (light blue) na Juba rangi ya bluu bahari lisilozidi vitanga vya mikono.

iv. Jozi mbili za viatu vyeusi vya kuchomeka vyenye visigino vifupi na jozi mbili za soksi nyeupe;

v. Tai ndogo ya rangi nyeusi (Butterfly tie)

**Sare kwa Wanachuo wa Kiume:**

i. Suruali mbili za rangi nyeusi zenye **mifuko mitatu tu** na zisizo za kubana wala kuchongwa. ***Suruali za jeans na mtumba haziruhusiwi*** **(Tazama mchoro ukurasa wa 6).**

ii. Mashati mawili ya mikono mirefu ya rangi ya bluu bahari (light blue) na koti jeusi la suit (kitambaa cha suruali na koti kisiwe na michilizi yeyote).

iii. Jozi mbili za viatu vyeusi vya kuchomeka na visivyo na visigino virefu na jozi mbili za soksi nyeusi;

iv. Tai ndefu ya rangi nyeusi.

**Mavazi ya Michezo kwa wote**

**i.** Tracksuit na bukta (light blue) na raba za michezo.

**ii.** T-shirt yenye nembo ya chuo inapatikana chuoni kwa gharama ya Tsh. 15,000/= tu.

NB: SARE HIZI ZITAKAGULIWA KABLA YA KUSAJILIWA.

## 6. MAAGIZO KUHUSU AFYA

Unatakiwa kuzingatia yafuatayo kwa ajili ya ustawi wa afya yako kwa kipindi chote cha mafunzo:

- Uje na fomu ya afya (**iliyoambatanishwa**) ikiwa imejazwa kikamilifu na Mganga wa hospitali inayotambuliwa na serikali, ili kuthibitisha hali ya afya yako.
- **NI LAZIMA** kuja na **kadi ya Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu yako yote kwa wenye bima za Afya.**
- Chuo **hakitoi** chakula maalum (Special diet)

## 7. MAWASILIANO

Mahitaji na maagizo yote yatakaguliwa wakati wa usajili. Kwa maelekezo zaidi unaweza kuwasiliana na Msajili wa Chuo kwa namba: **0766355937, 0713582172, 0621 013713; na kwa mahitaji ya Control number 0621013713.**

## 8. MWISHO

Jumuiya ya Chuo inatarajia kwamba utaonyesha tabia na mwenendo mwema na kuzingatia maelekezo ya walezi wako katika muda wote wa mafunzo yako kwani ***Ualimu Bora huanzia Chuoni***. Kauli mbiu ya Chuo chetu ni: **Mwalimu kwa Mfano.**

**Karibu Sana Chuo cha Ualimu Korogwe**

Hassan A. Ismail
**MKUU WA CHUO**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU KOROGWE
S.L.P 533 KOROGWE

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A**

Principal,

Korogwe Teachers' College,

P.O. Box 533

KOROGWE

**To the Medical Officer,**

..........................................

..........................................

..........................................

**RE: Mr/ Mrs/ Miss** ............................................................................

Please examine the above named to his/ her physical and mental fitness for a full time teacher education course. The examination should include the following categories (I - IV), each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of defect. Pregnancy (category iv) will also render a girl candidate ineligible for the course, including category V.

I. (a) Eyesight (b) Hearing (c) Speech (d) Limbs (e) Venereal disease (f) Leprosy

(g) Epilepsy (h) Epilepsy (i) Tuberculosis

II. Neuroses

III. Other serious diseases

IV. Pregnancy

V. Mental and Physical Fitness

NB: the applicant will not be admitted unless this is duly filled.

Date ............................................

Signature ....................................

**PART B** **MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/ she is physically fit / unfit and mentally fit / unfit to a fulltime teacher training course.

I . a) Eyesight ..........................................................................................

b) Hearing ..............................................................................................

c) Speech ..............................................................................................

d) Limb ..............................................................................................

e) Venereal Diseases ..............................................................

f) Leprosy ..........................................................

g) Epilepsy ..........................................................

h) Typhoid ..................................................

II. Neuroses

III. Other serious diseases


IV. Pregnancy

**Date** ................................................ **Signature** ..............................

**Station** ............................................ **Designation** ..........................


**KIAMBATANISHO NAMBA MOJA (1)**
**NB: SARE ZISIWE NGUO ZA MITUMBA.**

(a) Suruali



PICHA NA.1

(b) Sketi



PICHA NA.2

**MUHIMU:**

1. Mavazi yako kwa wakati wowote mwingine ni **LAZIMA** yaakisi maadili bora ya Ualimu. Nguo za kubana, pensi, vimini/vitop au zenye mipasuo mikubwa na mavazi angavu hayaruhusiwi.
2. Mwanachuo ambaye atakuja chuoni ***bila cheti halisi*** au ***result slip halisi*** ya kidato cha nne/astahahada (Cheti) ya Ualimu hatapokelewa **chuoni**.
3. Wasichana wanaruhusiwa kusuka nywele kwa mtindo wa twende kilioni nywele sizizozidi sita. ***Misuko ya rasta hairuhusiwi kabisa.***
4. Sare za **kuteleza/mtelezo (suruali/sketi)** na **mitumba** haziruhusiwi.